



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA KILIMO
BODI YA KOROSHO TANZANIA**



JARIDA LA KOROSHO KUANZIA NOVEMBA 15 - 30, 2022

VOL. 1 CBT.Na.0003
Imeandaliwa na:
Bodi ya Korosho Tanzania

WIZARA YA KILIMO BODI YA KOROSHO TANZANIA

1.0 UTANGULIZI

Biashara ya Korosho nchini Tanzania ipo katika wiki ya sita (6) tangu kuanza kwa minada tarehe 21 Oktoba, 2022. Biashara ya korosho imeendelea kufanyika ambapo hakuna mabadiliko makubwa ya bei za korosho. Aidha, wabanguaji wa ndani wameendelea kununua korosho kuitia soko la awali, ambapo mpaka kufikia tarehe 30 Novemba kiasi cha tani 110,292.598 zilikuwa zimenunuliwa.

2.0. MWENENDO WA SOKO KATIKA NCHI MBALIMBALI DUNIANI

2.1. MWENENDO WA SOKO AFRICA MAGHARIBI

Kwa mujibu wa mwenendo wa masoko katika nchi za India na Vietnam katika wiki mbili za mwisho wa mwezi Novemba, bei za korosho kutoka katika nchi za Afrika Magharibi kwa soko la India na Vietnam hauna mabadiliko makubwa ambapo korosho ghafi zimeuzwa kati ya dola za Kimarekani 1,250 hadi 1,300 kwa tani.

Aidha, katika nchi ya Guinea Bissau hadi mwishoni mwa mwezi Novemba, wamesafirisha nje ya nchi tani 158,000 kati ya tani 165,000 zilizoruhusiwa kusafirishwa nje ya nchi. Katika nchi ya Senegal hadi wiki ya mwishoni mwa mwezi Novemba, 2022 walikuwa na wastani wa tani 6,239 ambazo hazijauzwa na zimehifadhiwa katika ghala zikiendelea kuuzwa (Chanzo: Nkalo nuts). Mwenendo wa mauzo ya Korosho ghafi kutoka nchi za Afrika Magharibi kwenye soko la nje ni kama inavyoonekana katika jedwali na. I.

Jedwali Namba I

Nchi	Viwango vya Ubora	CIF-Bei/Tani wiki ilioishia 24/09/2022 (usd)	CIF-Bei/Tani wiki ilioishia 31/10/2022 (usd)	CIF-Bei/Tani wiki ya 05/11/2022 (usd)	CIF-Bei/Tani wiki ya 27/11/2022 (usd)
Nigeria/Ghana	46 - 47	1,150	1,170	0	0
Benin/Togo	45 - 46	1,150	1,150	1100	0
Cote d' ivore	46 - 47	1,080	-	1000 - 1050	1,000 - 1,100
Guinea Bissau/Senegal	50	1,420	1,280 - 1390	1300 - 1350	1,250 - 1,300

Chanzo: nkalo nut

2.2 Hali ya Zao nchini Msumbiji

Mauzo katika nchi ya Msumbiji tayari yameanza katika majimbo ya Nampula na Zambezi na korosho zinauzwa kati ya dola za Kimarekani 0.31 hadi 0.63 (Tshs. 722 hadi 1,468) kwa kilo (Chanzo: nkalo). Msumbiji inatarajia kuzalisha tani 150,000 kwa msimu 2022/2023 na wabanguaji wa ndani wanaruhusiwa kununua katika ngazi ya mkulima.

2.3. Hali ya Soko la Korosho Nchini India


Soko la ndani la korosho karanga katika wiki mbili za mwisho za mwezi Novemba, hazina mabadiliko na korosho karanga kwenda nje ya India zinazwa katika soko la nchi za Kiarabu pekee (UAE) ambapo bei zake si za kuvutia. Kupitia soko hilo, Bei ya korosho ghafi haina mabadiliko sana na korosho kutoka Tanzania zimeendelea kuuzwa kwa bei katika dola 1,300 hadi 1,400 (CNF) kwa tani (SHOT-52- 53). Huku korosho zilizosalia kutoka nchi za Ivory Coast na Benin zikiuzwa kwa dola za Kimarekani 1,100 kwa tani (SHOT- 47).

2.4. Hali ya Soko la Korosho katika Nchi ya Vietnam

Katika nchi ya Vietnam hakuna mabadiliko makubwa ya soko, kwani mahitaji ya korosho ghafi bado yako chini, kwa sababu wabanguaji wengi bado hawapokei mahitaji ya korosho karanga kutoka nchi za Ulaya. Katika miaka ya karibuni, nchi ya Vietnam imeonekana kuingiza kiasi kikubwa cha korosho ghafi kutoka nchi ya Cambodia, huku Cambodia ikiendelea kuongeza uzalishaji kutoka wastani wa tani 220,000 (2020) hadi kufikia wastani wa tani 650,000 (2022). Sababu kubwa ya ongezeko hili ikiwa ni upandaji wa mikorosho mipyä yenyé uwezo wa uzalishaji mkubwa kwa mti (Chanzo:ACA Global Market Encounter).

Jedwali Na.2: Bei za korosho ghafi katika nchi ya India na Vietnam kwa Novemba, 2022

MWENENDO WA BEI ZA WASTANI ZA KOROSHO GHAFI (RCN) DUNIANI-CASE STUDY YA INDIA NA VIETNAM KWA KIPINDI CHA SEPTEMBER HADI NOVEMBA, 2022		
TAREHE	BEI -CIF USD/TON	
	BEI YA CHINI	BEI YA JUU
September, 2022	1,080	1,390
02 Oktoba, 2022	1,080	1,350
31 Oktoba, 2022	1,050	1,280
05 Novemba, 2022	1,100	1,400
27 Novemba, 2022	1,000	1,400
SOT: 46 - 52		



Chanzo: nkalo nut & Cashewinformation

3.0 BEI ZA KOROSHO KARANGA KUTOKA NCHI MBALIMBALI

Bei ya korosho karanga katika nchi mbalimbali hutofautiana kwa kuzingatia kiwango cha uzalishaji, gharama za uzalishaji pamoja na teknolojia inayotumika kubangua korosho ghafi.

3.1. Bei Ya Korosho Karanga India Hadi Kufikia Wiki ya Mwisho Novemba, 2022

Hali ya bei ya korosho karanga kwa India ni kama inavyoonekana kwenye Jedwali Na. 3

**WIZARA YA KILIMO
BODI YA KOROSHO TANZANIA**

Jedwali Na. 3

BEI YA KOROSHO KARANGA INDIA HADI KUFIKIA WIKI YA MWISHO, NOVEMBA 2022					
MAELEZO YA DARAJA	DARAJA	Bei Dola/Kilo (FOB)		Bei TZS/Kilo (FOB)	
		Bei ya Chini	Bei ya Juu	Bei ya Chini	Bei ya Juu
White Whole Cashews 180	W180	12.87	14.09	29,703.96	32,519.72
White Whole Cashews 210	W210	10.05	11.27	23,195.40	26,011.16
White Whole Cashews 240	W240	8.95	9.73	20,656.60	22,456.84
White Whole Cashews 320	W320	7.84	8.27	18,094.72	19,087.16
Large White Pieces	LWP	7.11	7.35	16,409.88	16,963.80
Small White Pieces	SWP	6.37	6.86	14,701.96	15,832.88

Chanzo: Cashew information

3.2 Bei Ya Korosho Karanga Vietnam Hadi Kufikia Wiki ya Mwisho Novemba, 2022

Nchini Vietnam bado bei ya korosho karanga iko chini ukilinganisha na bei katika nchi zingine zinazobangua korosho. Jedwali Na. 5 linaonesha bei ya korosho karanga hadi kufikia mwishoni mwa mwezi Novemba, 2022.

Jedwali Na. 4

BEI YA KOROSHO KARANGA VIETNAM HADI KUFIKIA WIKI YA MWISHO, NOVEMBA 2022					
MAELEZO YA DARAJA	DARAJA	Bei Dola/Kilo (FOB)		Bei TZS/Kilo (FOB)	
		Bei ya Chini	Bei ya Juu	Bei ya Chini	Bei ya Juu
White Whole Cashews 180	WW180	7.93	8.15	18,302.44	18,810.20
White Whole Cashews 210	WW210	7.05	7.27	16,271.40	16,779.16
White Whole Cashews 240	WW240	5.84	6.17	13,478.72	14,240.36
White Whole Cashews 320	WW320	5.57	5.84	12,855.56	13,478.72
Large Pieces	LP	3.52	4.19	8,124.16	9,670.52
Small Pieces	SP	2.97	3.30	6,854.76	7,616.40

Chanzo: Cashew information

3.3 Bei Ya Korosho Karanga katika nchi za Afrika Hadi Kufikia Wiki ya Mwisho Novemba, 2022

Hadi kufikia mwanzoni mwa mwezi Novemba, bei ya korosho karanga kwa nchi za Afrika Magharibi ambazo ni Ivory Coast, Ghana, Benin nk. inakadiriwa kuwa kama inavyoonekana kwenye Jedwali Na.5

Jedwali Na.5

BEI YA KOROSHO KARANGA AFRIKA MAGHARIBI HADI KUFIKIA WIKI YA MWISHO, NOVEMBA 2022					
MAELEZO YA DARAJA	DARAJA	Bei Dola/Kilo (FOB)		Bei TZS/Kilo (FOB)	
		Bei ya Chini	Bei ya Juu	Bei ya Chini	Bei ya Juu
White Whole Cashews 210	W210	7.718	8.048	17,811.99	18,574.78
White Whole Cashews 240	W240	6.278	6.608	14,489.62	15,251.26
White Whole Cashews 320	W320	5.617	6.057	12,964.04	13,979.56
White Whole Cashews 450	W450	5.066	5.507	11,692.33	12,710.16
White Splits	WS	4.626	4.736	10,676.81	10,930.69
Large Pieces	LP	3.414	3.634	7,879.51	8,387.27
Small Pieces	SP	2.643	2.863	6,100.04	6,607.80

Chanzo: Cashew information

**WIZARA YA KILIMO
BODI YA KOROSHO TANZANIA**

3.4. Bei Ya Korosho Karanga Tanzania Zinazouzwa Nje Ya Nchi Hadi Kufikia Wiki ya Mwisho Novemba, 2022

Bei ya korosho karanga zinazobanguliwa na wabanguaji wa ndani na kuuzwa nje katika nchi za Uhlanzi, Uturuki, Misri, nchi za Uarabuni nk. ni kama inavyoonesha kwenye Jedwali Na. 6


Jedwali Na.6

BEI YA KOROSHO KARANGA TANZANIA ZINAZOUZWA NJE HADI KUFIKIA WIKI YA KWANZA NOVEMBA, 2022			
MAELEZO YA DARAJA	DARAJA	Bei ya Dola & Tzs/Kilo (FOB)	
		Bei ya Dola/Kilo	Bei Tzs/Kilo
White Whole Cashews 180	W180	8.50	19,618.00
White Whole Cashews 240	W240	7.70	17,771.60
White Whole Cashews 320	W320	7.20	16,617.60
White Splits	WS	5.50	12,694.00

Chanzo: TACP

Jedwali Namba 7: Uwiano Wa Bei Daraja WW320

UWIANO WA BEI DARAJA LA WW320 FOB		
Nchi	Bei Dola/Kilo	Bei Tzs/Kilo
Vietnam	5.84	13,478.72
India	8.25	19,087.16
Afrika Magharibi	6.06	13,979.56
Tanzania	7.20	16,617.60



4.0 MWENENDO WA ZAO LA KOROSHO NCHINI TANZANIA

4.1 Mwenendo wa minada

Hadi kufikia tarehe 30 Novemba, 2022, wastani wa tani 126,184 tayari zimekusanya katika ghalaa za minada na kati ya hizo tani 110,292.598 tayari zimeuzwa zenye thamani ya shilingi 208,966,391,392 Minada ya Mauzo ya Korosho bado inaendelea katika maeneo mbalimbali nchini, huku bei ya chini ikiwa imeshuka kwa asilimia 5.5 kutoka wiki iliyoishia tarehe 15 Novemba ambapo bei ya chini ilikuwa Tshs. 1,810 kwa kilo. Bei ya juu bado haina mabadiliko makubwa ambapo imeshuka kwa asilimia 0.8 katika wiki iliyoishia tarehe 27 Novemba, 2022 ambapo bei ya juu ilikuwa Tshs. 2,012 kwa kilo. Mahitaji ya korosho ghafi katika nchi wanunuzi yameegemea sana katika ubora wa kuanzia SHOT 50 hadi 54 huku uzalishaji nchini ukiwa na madaraja mawili ambayo ni daraja la kwanza (SHOT 48 hadi 54) na daraja la pili (SHOT 44 hadi 47). Wakulima wanaendelea kushauriwa kuuza korosho zao kwa kuzingatia bei zilizopo kwa sasa katika nchi wabanguaji wakubwa (India na Vietnam).



**WIZARA YA KILIMO
BODI YA KOROSHO TANZANIA**

Jedwali Na. 8a: Mwenendo wa minada ya korosho kuanzia 16 hadi 20 Novemba, 2022

MWENENDO WA MNADA WA KOROSHO GHAFI KUANZIA TAREHE 16/11/2022 HADI TAREHE 20/11/2022						
NA	TAREHE	CHAMA KIKUU	KIASI (kgs)	BEI YA MAUZO (Tshs)		THAMANI (Tshs)
				BEI YA CHINI	BEI YA JUU	
1	16/11/2022	CORECU	1,854,644	1,981	1,900	3,512,618,123
2	17/11/2022	TAMCU	1,667,561	1,855	1,890	3,104,837,780
3	18/11/2022	MAMCU	9,298,360	1,862	2,005	17,979,569,419
4	18/11/2022	TANECU	6,880,026	1,930	2,001	13,439,541,463
5	19/11/2022	LINDI MWAMBAAO	1,710,102	1,835	1,842	3,142,138,818
6	20/11/2022	RUNALI	5,031,111	1,950	1,982	9,888,660,447
JUMLA KUU			26,441,804	1,835	2,005	51,067,366,050

Jedwali Na. 8b: Mwenendo wa minada ya korosho kuanzia 23 hadi 27 Novemba, 2022

MWENENDO WA MNADA WA KOROSHO GHAFI KUANZIA TAREHE 23/11/2022 HADI TAREHE 27/11/2022						
NA	TAREHE	CHAMA KIKUU	KIASI (kgs)	BEI YA MAUZO (Tshs)		THAMANI (Tshs)
				BEI YA CHINI	BEI YA JUU	
1	23/11/2022	CORECU	1,273,813	1,720	1,860	2,335,719,013
2	24/11/2022	TAMCU	2,345,129	1,820	1,822	4,277,709,250
3	25/11/2022	MAMCU	6,184,241	1,860	1,990	11,993,995,676
4	25/11/2022	TANECU	4,712,635	1,930	1,995	9,149,622,962
5	26/11/2022	LINDI MWAMBAAO	1,282,741	1,710	1,757	2,225,545,200
6	27/11/2022	RUNALI	4,777,795	1,960	1,985	9,415,448,713
7	29/11/2022	UKICU	117,319	-	1,720	201,788,680
JUMLA KUU			20,693,673	1,710	1,995	39,599,829,494

5.0 UHAMASISHAJI MATUMIZI NA UWEKEZAJI KATIKA BIDHAA ZA KOROSHO NCHINI

Uongezaji thamani katika zao la korosho ndio njia pekee ya kuleta tija katika zao la korosho na kuongeza kipato kwa mkulima na Taifa kwa ujumla. Hivi karibuni kumekua na hamasa kubwa katika uongezaji thamani wa bidhaa zitokanazo na zao la korosho kama vile uzalishaji wa siagi ya korosho, maziwa ya korosho, sharubati, mvinyo, n.k. Uwepo wa bidhaa hizi sokoni utasaidia uhamasishaji wa matumizi yake na hivyo kupanua wigo wa soko na usindikaji bidhaa zingine za korosho badala ya kutegemea korosho karanga pekee. Bodi inaendelea kutoa elimu ya utengenezaji wa bidhaa hizi kwa kushirikiana na Taasisi mbalimbali pamoja na wasindikaji ambao tayari wameanza kuwekeza katika mnyororo wa zao la korosho. Utengenezaji rahisi wa siagi ni kama inavyoonekana katika sehemu ya 5.1.

5.1 Jinsi ya Kutengeneza Siagi ya Korosho (Cashew Butter)

Siagi ya korosho hutengenezwa kwa korosho zilizookwa au kukaangwa kwa mafuta. Kijiko kimoja cha siagi ya korosho (isiyotiwa chumvi) hutoa kalori 94 na asilimia 12% ya mafuta yanayohitajika mwilini kwa siku moja. Mafuta yatokanayo na Korosho ni mazuri kwa afya kwa sababu hayana lehemu (Cholesterol) ukilinganisha na mafuta yatokanayo na bidhaa nyingine.

Hatua I.

- ◊ Chukua kiasi cha korosho ulizokwisha kuziandaa kwa kuoka au kukaanga. Mara nyingi inashauriwa kutumia korosho vipande ili kuviongezea thamani.
- ◊ Saga kwa kutumia mashine maalum ya kusagia vyakula ama mashine yenye nguvu ya kusagia vyakula nyumbani (High Power Blender).
- ◊ Ongeza kiwango kidogo cha mafuta ya kula kurahisisha usagaji. Korosho ina kiwango kidogo sana cha mafuta ukilinganisha na karanga nyingine,

**WIZARA YA KILIMO
BODI YA KOROSHO TANZANIA**

Hatua ya 2

- ◊ Chukua rojo la korosho uliyosaga kwa hatua ya kwanza kisha unaweza ongeza ladha unayoipenda kama vile, Chocolate, strawberry, vanilla, n.k ama ukaiacha na ladha asilia.
- ◊ Waweza ongeza kiuanganishi “Stabilizer” ili mafuta yasijitenge na siagi
- ◊ Saga tena kwa dakika 15 – 20 kwa kutegemea na aina ya mashine unayotumia, kisha acha ipoe kwa masaa mawili.
- ◊ Baada ya hapo unaweza fungasha na tayari kwa matumizi.



Chanzo: Akros Limited



**MAWASILIANO
MKURUGENZI MKUU
BODI YA KOROSHO TANZANIA
S.L.P 533 TANU ROAD – MTWARA
Simu: +255 (23) 233 3303/233 3450
Barua pepe: info@cashew.go.tz
Tovuti: www.cashew.go.tz**